# MAOMBI YA TETEMEKO

***“ Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa WAKIMWOMBA Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza. Ghafula pakawa TETEMEKO KUU LA NCHI, hata misingi ya gereza IKATIKISIKA, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vya wote vikalegezwa.”***
***[MATENDO 16:25-26].***

***“…Basi yule akida, na hao waliokuwa pamoja naye wakimlinda YESU, walipoliona TETEMEKO LA NCHI na mambo yailiyofanyika, WAKAOGOPA SANA wakasema, HAKIKA HUYU ALIKUWA MWANA WA MUNGU***
***[MATHAYO 27:54].***

***“ Hata walipokwisha KUMWOMBA Mungu, mahali pale walipokusanyika PAKATIKISWA [NA TETEMEKO], wote wakajaa ROHO MTAKATIFU, WAKANENA NENO la Mungu kwa ujasiri.”***
***[MATENDO 4:31 ]***

**JUSTICE B. LUTASHOBYA**

# MAOMBI YA TETEMEKO

***Copyright 2010:***
***Mchungaji Justice B.Lutashobya***
***Revised 2014***

***Design by: LIBERTY MEDIA CO.LTD***
***Cell: + 255 717 599958 / 767 599958***
***Email: liberty.co12@gmail.com***

***Kimechapwa Tanzania Na:***
***Prosper Printing Company (PPC)***
***S.L.P. 72635, Dar-es-Salaam***
***Meneja: +255-715-964536; +255-756-964536***
***Barua pepe: fadhilijuliasi@gmail.com***

***Chapa ya kwanza mwaka 2010***
***Chapa ya Pili mwaka 2014***

***Haki zote zimehifadhiwa***
***Hairuhusiwi kunakili kitabu hiki***
***kwa namna zozote bila ruhusa ya Mwandishi***
***kwa ajili kuuza au kufanyia biashara.***

***Lakini unaruhusiwa kunakili***
***Sehemu tu ya ujumbe katika kitabu hiki***
***Kwa ajili ya Kushuhudia, kuhubiri na kufundisha wakristo***
***Na wasio wakristo, kanisa lolote, shule za jumapili,***
***shule za huduma Mikutano ya injili, semina ya neno la Mungu Na***
***madarasa ya maombi.***

***Maandiko yote ni kutoka katika Biblia tafsiri ya Union version,***
***isipokuwa kama imetajwa vinginevyo.***



# SHUKRANI

Mungu wa Mbinguni, ninakushukuru katika Jina la Yesu na la Roho Mtakatifu uliyenihuisha kuandika kitabu cha MAOMBI YA TETEMEKO; kwa watu wako uliowaumba kwa mfano wako. Ufalme wako uje juu watu wako kupitia Neno lako lililotumwa kwao ili kuwaokoa na kuwaponya kutoka maangamizo yao. Ushuhuda wa Injili ya Yesu Kristo kwa ufunuo, ushauri , mafundisho na kumbukumbu za Roho Mtakatifu ndiyo uliyofanikisha maandalizi ya kitabu hiki katika nafasi ya kwanza. Heshima na Utukufu namrudishia BWANA WA MAJESHI KATIKA KITI CHA ENZI. Pili natoa shukrani kwa Mke wangu mpendwa Adeline Lutashobya kwa kujitolea kwake kuhakiki kitabu hiki kama mhariri, akiongozwa na Roho Mtakatifu. Ahsante kwa maombi ya mapinduzi uliyofanya kuhakikisha kitabu hiki kinatoka katika uvuvio wa Roho Mtakatifu. Tatu nawashukuru shemeji yangu Anchila na watoto wangu wapendwa, Jesse, Joyous, Joyce na Namala ambao waliendelea kuiombea kazi hii ya mapinduzi, kuhakikisha inatimizwa. Mungu wa Mbinguni awafungulie Milango 12 ya mapinduzi katika maisha yenu. Nne, Namshukuru Maro Nyamate aliyetoa ushauri wa kina katika haki za kitabu hiki, pamoja na sadaka ya muda wake kuunda tovuti na barua pepe za huduma ya WMMC na BLESSING COMMUNITY. Mwisho namshukuru Robert Mwasongwe ambaye amesaidia kutengeneza sehemu ya jarada ya kitabu hiki pamoja na kukipanga katika mfumo wa kutolewa chapa.

**NEEMA YA BWANA WETU YESU KRISTO, NA UPENDO WA MUNGU BABA, NA USHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU, UWE PAMOJA NASI SOTE , SASA NA HATA MILELE. AMINA**

# YALIYOMO

SHUKRANI.......... III
UTANGULIZI.......... IX

**SURA YA KWANZA.......... 1**
***SAFARI YA KWENDA KWENYE .......... 1***
MAOMBI .......... 1
Hatua za safari kupeleka Maombi kwa Mfalme wa Wafalme.......... 3
Hatua ya kwanza: Rangi ya Udongo au Njano:.......... 5
Hatua ya pili: Rangi ya Kijani.......... 6
Hatua ya tatu: Rangi Nyekundu.......... 7
Hatua ya nne: Rangi ya Bluu.......... 8
Hatua ya tano: Rangi ya Zabibu.......... 9
Hatua ya sita: Rangi ya Nyeupe.......... 9
Wakati wa kuongea na Shetani katika Maombi.......... 12

**SURA YA PILI.......... 17**
***MAOMBI YA TETEMEKO.......... 17***
Neno la Maombi.......... 21
Sauti na Lugha ya Maombi.......... 24
Ishara za Maombi.......... 31
Roho wa Maombi.......... 32
Hupanda Mbegu ya Maombi.......... 33
Hutupa uwezo wa kumuita Baba katika maombi.......... 33
Hufunua jambo la Kuomba.......... 34
Huomba ndani yako.......... 35
Hutupa maono na uwezo kupambanua roho.......... 35
Huachilia roho ya Imani.......... 35
Hutufundisha kuomba katika roho na lugha ya maombi.......... 36
Hutupa upako wa kupigana vita katika roho.......... 36
Aina za Maombi.......... 36

**SURA YA TATU.......... 45**
***MAOMBI YA VITA.......... 45***
Jinsi ya kuomba Maombi ya hatari na vita. Usipige magoti ... unapoomba maombi haya:.......... 49
Maana ya Maombi ya Vita.......... 51
MIFANO WA MAOMBI YA VITA KWA KUKIRI NENO.......... 57
UKIRI WA MUNGU.......... 57
UKIRI WA NGUVU.......... 58
UWEZO KATIKA ULIMI WAKO.......... 59

PIGANA NA UWE HURU SASA ........ 60
Uwepo wa Bwana ........ 60
ROHO MTAKATIFU ........ 60
WARUHUSU MALAIKA WA VITA ........ 61
DAMU YA YESU KRISTO ........ 61
FUNGA MAPEPO YOTE YANAYOZUIA MAOMBI ........ 61
UKUNGU WA KIPEPO ........ 62
JIFUNGUE (JIWEKE HURU) ........ 62
TELEVISHENI (LUNINGA) ZA KIPEPO ........ 63
FUNGA FALME NA MAMLAKA ........ 65
MANENO MACHAFU YOTE ........ 65
MALI ZA MASHETANI ........ 66
VIFUNGO VYA (MOYO NAFSI NA MAWAZO) ........ 66
DHAMBI ZA MABABU ........ 67
DHAMBI AU LAANA ZA WAHENGA (WAKALE) ........ 68
KUTOKA KWAKO MWENYEWE ........ 69
KWA KUTOMTII MUNGU ........ 69
KUTOKA KWA SHETANI NA WAJUMBE WAKE ........ 69
LAANA YA NCHI YA TANZANIA ........ 70
AINA YA MAKUBALIANO ........ 71
MASHAMBULIZI YA NDOTO ........ 71
SHEREHE ZA MIJI NA MILA ZA KIFAMILIA ........ 72
ULINZI WA KIPEPO ........ 72
JITENGE MWENYEWE ........ 73

**SURA YA NNE ........ 75**
***MAOMBI YA KUSHINDANA ........ 75***
MUSA alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana. ........ 76
JOSHUA alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana : ........ 77
DANIEL alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana. ........ 78
SHADRAKA, MESHAKI NA ABNEGO walisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana ........ 81
ESTA alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana. ........ 83
SAMSONI alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana: ........ 84
ELIYA alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana: ........ 85
YESU KRISTO alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya ... kushindana: ........ 86
Mtume PAULO alisababisha TETEMEKO kwa maombi ya ... kushindana: ........ 89
KANISA LA YERUSALEMU lilisababisha TETEMEKO kwa maombi ya kushindana. ........ 90

**SURA YA TANO ........ 93**
***MAOMBI YA MAANGAMIZI ........ 93***
Mfano wa Maombi ya Maangamizi ........ 96
WARUHUSU MALAIKA WA VITA! ........ 96
TUMIA DAMU YA YESU KRISTO ........ 96
FUNGA MAPEPO YOTE YANAYOZUIA MAOMBI YAKO... 96

**SURA YA SITA ........ 99**
***MAOMBI YA ZIMA MOTO ........ 99***

**SURA YA SABA ........ 103**
***MAOMBI YA KUFUNGA ........ 103***
MUSA alisababisha tetemeko kwa kufunga na kuomba... 104
ESTA alisababisha tetemeko la nchi kwa kufunga na Kuomba. ........ 107
ELIYA alisababisha tetemeko nchini Israeli kwa kufunga na Kuomba. ........ 109
MAOMBI YA MAANGAMIZI ........ 109
YONA alisababisha tetemeko katika mji wa Ninawi kwa Injili ya kufunga na Kuomba ........ 110
YESU alisababisha tetemeko mbinguni, duniani na kuzimu kwa kufunga na kuomba. ........ 115
MAOMBI YA ZIMA MOTO ........ 115
PAULO alisababisha tetemeko katika bara la Asia na Ulaya kwa Injili ya kufunga na Kuomba. ........ 116
MASHAHIDI WAWILI WA SIKU ZA MWISHO watasababisha tetemeko duniani kwa Kufunga na kuomba: ........ 119

**SURA YA NANE ........ 123**
***KUOMBA KWA LUGHA ........ 123***

**SURA YA TISA ........ 127**
***MAOMBI YA SIFA ........ 127***

**SURA YA KUMI ........ 131**
***MAOMBI YA MAOMBOLEZO ........ 131***
MAOMBI YA KUFUNGA ........ 131

**SURA YA KUMI NA MOJA ........................................ 137**
***MAOMBI YA MKESHA........................................ 137***
Bwana Yesu ALIKESHA.................................................... 138
Mitume 12 na Mtume Paulo WALIKESHA........................ 139
KUOMBA KWA LUGHA .................................................... 141

**SURA YA KUMI NA MBILI......................................... 143**
***MAOMBI YA MSALABA...................................... 143***
MAOMBI YA SIFA ............................................................ 145
MAOMBI YA MAOMBOLEZO .......................................... 149
USHUHUDA WA MAOMBI YA MSALABA YA BLESSITT:. 150
MAOMBI YA MAOMBOLEZO .......................................... 151
Kuhusu Maombi:............................................................... 152
Unaweza sasa kuomba maombi kwa ajili ya: .................. 152
Maombi ya Baraka........................................................... 153
“Maombi ya Uponyaji”...................................................... 153
“ Maombi ya Upako na Uweza” ....................................... 154
“Maombi ya Wokovu”! ..................................................... 155
MAOMBI YA MKESHA..................................................... 155

**SURA YA KUMI NA TATU .......................................... 157**
***MAOMBI YA UFUNUO......................................... 157***
MAOMBI YA MKESHA..................................................... 157

**SURA YA KUMI NA NNE........................................... 161**
***TAMATI................................................................. 161***
MAOMBI YA MSALABA.................................................... 161
KWANZA: Kujenga roho ya Imani kwa Kusikia................ 163
MAOMBI YA MSALABA.................................................... 163
PILI: Kutenga Nuru na Giza.............................................. 166
TATU: Kufanya Urejesho .................................................. 167
NNE: Hukumu ya maadui wa Kanisa ............................... 168
TANO: Mapinduzi ya Kiroho; Kiuchumi na Kisiasa ........... 171
UNABII HUU LAZIMA UTIMIE!......................................... 171
MAOMBI YANGU YA TETEMEKO..................................... 173



# UTANGULIZI

***“ Hata walipokwisha KUMWOMBA Mungu, mahali pale walipokusanyika PAKATIKISWA[ NA TETEMEKO], wote wakajaa ROHO MTAKATIFU, WAKANENA NENO la Mungu kwa ujasiri.”***
***[ MATENDO 4:31 ]***

***“ Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa WAKIMWOMBA Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza. Ghafula pakawa TETEMEKO KUU LA NCHI, hata misingi ya gereza IKATIKISIKA, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vya wote vikalegezwa.”***
***[MATENDO 16:25-26].***

Karibu kwenye uwanja wa mkutano wa Maombi ya tetemeko kwa njia ya kitabu hiki ulichonacho mkononi mwako. Roho wa maombi ataanza kukuonyesha mambo makubwa usiyoyajua, na utajikuta tayari unajaa nguvu za kuomba bila kukoma. Sasa mbingu zimefunguka juu yako, utakapoanza kusoma kitabu hiki; roho yako itaanza kupokea mafuta kutoka mbinguni yatakayofanyika kilipuaji katika maombi yako ya tetemeko juu ya utawala wa shetani. Utaanza kuona siri za shetani, utaanza kuona maadui zako, utaanza kuona majeshi ya kipepo yanayojiandaa kukufaidhaisha katika familia yako, mtaani kwako, kijijini kwako, kwenye kata yako, tarafa yako, wilaya yako, mkoa wako na taifa lako. Lazima utainuka kwa ajili ya kupigana vita ya kiroho dhidi upinzani ambao umeandaliwa siku

nyingi ila ulikuwa ujajua bado! Kumbe FAMILIA YAKO IMEVAMIWA! KUMBE MTAA WAKO UMEVAMIWA! KUMBEA KIJIJI CHAKO KIMEVAMIWA! KUMBE KATA YAKO IMEVAMIWA! KUMBE TARAFA YAKO IMEVAMIWA! KUMBE WILAYA YAKO IMEVAMIWA! KUMBE MKOA WAKO UMEVAMIWA! KUMBE TAIFA LAKO LIMEVAMIWA! CHUKUA HATUA YA KUSHIKA SILAHA YAKO MKONONI INAYOITWA MAOMBI YA TETEMEKO! Naomba ukumbuke kuwa maombi ni vita, kwahiyo vita vyote vya kiroho na kimwili vinahitaji JESHI, SILAHA, VYOMBO VYA JESHI KAMA NDEGE, MAGARI NA VIFARU; na pia vita vinahitaji fedha. Msomaji wangu shalom, najua unajua vizuri juu ya vita ulinayo, vita ya kifamilia, vita ya kifedha, vita ya watoto, vita ya ndoa yako, vita ya wokovu, vita ya afya yako, vita ya kazi yako, vita ya kilimo chako, vita ya uongozi wako wa kijiji, kata, wilaya, mkoa na hata vita ya kitaifa katika nchi yetu Tanzania. Kitabu hiki kinakuletea ujumbe wa silaha utakayotumia na jinsi ya kuitumia, hiyo silaha ya maombi na kisha upate ushindi asilimia 100% kwa kuitetemesha ngome ya yule mwovu.

Maombi ni mazungumzo kati ya Watu na Mungu au Kati ya wasioamini na shetani. Maombi ni mkutano wa kivita ambao wajumbe wake ni wakristo waombao na Mungu ndiye mwandaaji wa mkutano; anayesaini vita kwa Jina la Yesu; ndiye aliyekabidhi vifaa vya jeshi la maombi na ndiye anayeongoza vita kwa Roho wa Maombi. Maombi ni MKUTANO WA KIFALME, kati ya MFALME NA WAFALME WADOGO PAMOJA NA WATU WENGINE KATIKA UFALME WAKE. Maombi ni safari ya kutoka katika ENEO LA CHINI KWENDA JUU KATIKA ULIMWENGU WA ROHO; KUTOKA DUNIANI KWENDA KATIKA KITI





CHA MFALME WETU YESU ALIPO, KATIKA HEKALU LA MBINGUNI. KWA SABABU SISI TUKO CHINI YA UFALME WAKE, NDIYO TUNAPASWA KUOMBA APOINTIMENTI YA KUKUTANA NAYE, KATIKA HEKALU LA KIFALME LILILOKO MBINGUNI. Mtu yeyote anapoanza kumtafuta Mungu kwa maombi kuna kusudi la kumtafuta; KABLA HUJAFIKA KATIKA GETI LA KUINGIA MAHALA PATAKATIFU PA PATAKATIFU KWA AJILI YA MKUTANO NA MFALME KUNA NGAZI NYINGI INABIDI UZIPITIE KUPELEKA MSTAKABARI WA MAOMBI.

TETEMEKO, TETEMEKO, TETEMEKO! Tetemeko la Maombi linakuja Tanzania na litafunika anga, bahari na nchi kavu katika miji yote Tanzania. Litapindua pindua Serikali za Mitaa, Wilaya, Mikoa, Manispaa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara zote, Sekta ya uma na binafsi, mashirika ya uma na binafsi, miundo mbinu ya Taifa na Serikali kuu ya Jamhuri ya Muungano zitapigwa na TETEMEKO KUU LA MAOMBI. TAMKO LA UNABII KWA KINYWA CHA NABII EZEKIEL, LITAIKUMBA TANZANIA NA VITONGOJI VYAKE! HATA KAMA HUAMINI KATIKA MANABII WA KITANZANIA, LAKINI LAZIMA MAPENZI YA MUNGU YATIMIZWE KWA TANZANIA! MITUME, MANABII, WAINJILISTI, WACHUNGAJI NA WAALIMU FANYA HARAKA MKAWAANDAE WATANZANIA, KABLA YA TETEMEKO WAPATE YUMKINI KUPONA. KAMA ISRAELI INAVYOANDALIWA NA UNABII WA EZEKIELI JUU TETEMEKO LITAKALOWAKUMBA MAGOGU NA GOGU, MAADUI WA ISRAELI,UNABII HUU UNAKUJA TANZANIA. MAOMBOLEZO YA WATANZANIA YAMESIKIKA JUU MBINGUNI, MUNGU AMEANDAA TETEMEKO KULIOKOA KANISA LA TANZANIA NA

MAADUI WA ROHONI NA MWILINI.

Tanzania mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya, Tarafa kwa tarafa, kata kwa kata, kijiji kwa kijiji na kitongoji kwa kitongoji, itatikiswa, na masikio yatawasha, na kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri kuwa YESU KRISTO NI BWANA. Kabla ya kurudi kwa Yesu Kristo mara ya pili, dalili zimekwisha anza kuonekana, TETEMEKO JUU YA MIOYO YA JIWE, MIAMBA MSHAPO, MIAMBA MIGUMU NA MIAMBA MOTO, LITAITIKISA TANZANIA KWA MARA NYINGINE TENA, NA ITAKUWA ATAKAYELIITIA JINA LA BWANA ATAOKOKA.

***“..ambaye SAUTI yake ILIITETEMESHA nchi wakati ule; lakini sasa amehaidi akisema, Mara moja tena NITAITETEMESHA SI NCHI TU, bali na MBINGU pia. Lakini neno lile Mara moja tena, ladhihirisha KUHAMISHWA vile viwezavyo KUTETEMESHWA, kama vitu vilivyoumbwa, ili vitu visivyoweza KUTETEMESHWA VIKAE.” [WAEBRANIA 12: 26-27].***

Mungu mkuu anatisha sana, hasa tukikumbuka matetemeko yaliyopita tangu alipoziumba mbingu na nchi. Watu wengi kwa sababu ya shughuli nyingi za kukimbizana na mkate wa kila siku, hawana muda wa kumtafakari Mungu kisha kumwabudu. Mungu tangu mwanzo anapenda kudumisha mawasilino mazuri na mwanadamu, lakini shetani alipofanya pando la dhambi, mawasiliano yakakatika kwa muda. Dhambi ni mlango unaofunga mawasiliano kati ya Mungu na Kanisa; Wakristo wanahitaji kuchukua shoka la moto na upanga wa moto (Waefeso 6:17); kuvunja mlango huu unaolitesa Kanisa tangu 1980. Dhambi ikakaa sana





nyumbani mwa Bwana inakuwa kama laana, wakristo wadogo kwa wakubwa wanarithi. Bado Bwana YESU ALITUMWA KURUDISHA UHUSIANO NA MUNGU MKUU, akafanya upatanisho kwa njia ya MSALABA. KATIKA MSALABA NA KATIKA KUFANYA UPATANISHO, BWANA YESU kwa NENO, MAOMBI PAMOJA NA KULIA SANA NA MACHOZI, TETEMEKO LA MAOMBI LILITIKISA PALE KALVARI. Shetani alitetemeshwa na kuchanganyikiwa kuona AGANO JIPYA LINATOBOZA; HALELUYA! Maana alijua mateka wa Mungu HAWATAKOMBOLEWA, na sasa bomu kali limepigwa kwa kishindo kikubwa na kuitetemesha dunia na kuzimu. Giza lilifunika nchi, Mungu akaanza kuwasiliana na wanadamu, kwa ishara hii ya giza, Mungu akaonyesha kuwa wanadamu wamejaa dhambi. Bwana Yesu alithibitisha kuwa Dunia imejaa dhambi! Baada ya ishara hii ya giza, **SAUTI YA ELOI, ELOI LAMASABAKTHANI** ilifuata kama kombora la ATOMIKI, lililopiga toka mbinguni, hadi kuzimu, kupasua miamba na kufunua makaburi!

***“Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi. Na kama saa tisa, YESU akapaza SAUTI yake kwa nguvu akisema ELOI, ELOI, LAMASABAKTHANI? yaani, Mungu Wangu Mungu wangu, mbona umeniacha?. [ MATHAYO 27: 45-46 ]. Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; NCHI IKATETEMEKA; miamba ikapasuka; MAKABURI YAKAFUNUKA; ikainuka MIILI MINGI YA WATAKATIFU WALIOLALA. nao wakiisha kutoka makaburini mwao, BAADA YA KUFUFUKA KWAKE, wakaingia MJI MTAKATIFU, wakawatokea wengi wengi. [MATHAYO 27:51-54].***

Tunapotazama kizazi hiki ni kizazi cha siku za mwisho, ambacho YOHANA MBATIZAJI alikiita kizazi cha nyoka; kinahitaji INJILI YA TETEMEKO ili kukinusuru na jehanamu ya moto. Biblia inasema kimejaa MIOYO YA JIWE, roho za watu hawa shetani amezifanya kuwa MIAMBA MSHAPO, MIAMBA TABAKA NA MIAMBA MOTO! Miamba kama hii inahitaji TETEMEKO la baruti kali, ya MOTO MKALI ili ipate kupasuka na kulainika. Mara nyingi miamba ikishapasuliwa, inatakiwa kumwagiwa maji KUIPOZA kwa ajili ya matumizi. Kwa sababu ya TETEMEKO KALI, mioyo ya miamba hujawa na hofu na kutetemeka sana, kwa sababu ya kusikia milipuko katika kupasua miamba. Hofu ya Mungu inaingia ndani ya mioyo kama hii, ndipo huanza KUMWAMINI Mungu, kisha KUTENGWA na dhambi, na hatimaye kupokea WOKOVU. Katika nchi yetu, watu wengi Tanzania mara nyingi husema mtu akiokoka lazima amepatwa na tatizo, ndiyo lilimtokea TETEMEKO, NA KWAKO LINAKUJA! UWE TAYARI! HALELUYA! Lakini ukitii Roho Mtakatifu, Mungu hana haja ya kutuma tetemeko liongee na wewe.

Masomo yote katika kitabu hiki yatakupeleka HATUA KWA HATUA, hadi kwenye ufunuo halisi wa mwandishi. Na kila hatua utakayofikia, Roho Mtakatifu namuomba akusaidie kufikia maandalizi ya kujiweka tayari kupokea nguvu itakayokuwezesha kupona na kubaki salama wakati Tetemeko litakapopita. Kwamba hata ukisikia mlipuko ndani ya tetemeko la kiroho na mwili ujue ni wapi pa kukimbilia UPATE KUOKOKA. Maana tetemeko likitokea ghafula watu hukimbia ovyo, wanaziacha familia zao, huchanganyikiwa, hata waganga huchanganyikiwa,





wanasayansi, wanafalsafa, wakuu wa nchi, wakuu wa dini, wakuu wa giza na mifumo yote huchanganyikiwa, wakati huo wakitafuta wafanye nini. Pale Kalvari giza lilipoanza kufunika nchi, Waandishi, Wanasheria, Wakuu wa dini na makuhani, Mafarisayo na Masudukayo, pamoja na wakuu wa nchi, walichanganyikiwa wakaanza kukimbilia majumbani. Mbinguni tetemeko lilifika, na pazia la hekalu likapasuka; Duniani Miamba ilipasuka na makaburi kufunuka; Kuzimu wafu walifunguliwa na kukombolewa na kuhamishiwa katika mji Mtakatifu PARADISO. Tetemeko la KIROHO linatisha zaidi ya tetemeko la ardhi hapa duniani, maana MBINGUNI KUNATIKISIKA, NA KUZIMU KUNATETEMEKA.

Kitabu hiki kimeandikwa pia kutoa wito wa kuandaa MOYO WAKO, ili upate kufaidika katikati ya tetemeko kuliko kupata hasara. Maana kabla Mungu hajafanya uamuzi kuleta tetemeko, HUTOA MAONYO KUPITIA MANABII WAKE. Na kama wewe ni MWAMINI, MWANAFUNZI NA MTUME, uwe sehemu ya tetemeko hili kwa kupeleka MAOMBI YA TETEMEKO YA YESU KRISTO katika miji na vijiji vilivyoko Tanzania, ambako kuna mioyo ya miamba migumu na jeuri. Ukiruhusu MIRIJA ya mafuta kunyonya mafuta kutoka milimani, KWA KUFUNGA NA KUOMBA na KANISANI kwenye NENO LA MUNGU, kisha ipeleke miambani, utaichomeka kwenye mawe magumu [ MIOYO], na kisha lipua moto, mapepo yatakimbia kwa sababu ya mlipuko mkali, mawe yatavunjika vipande vipande, kisha yatulize kwa maji. Kanisa ni kituo cha UMISHENI; NI KITUO CHA MRADI WA KUSAMBAZA MAFUTA NA MAJI kwenda eneo la kupasua miamba. Baada ya tetemeko hili la kupasua miamba, watu WENGI WATAOKOLEWA,

baada ya kukimbilia kwa YULE ALIYEUMBA TETEMEKO, yaani YESU KRSITO. Lakini lazima watatetemeka, lazima watamwabudu na lazima watamsifu, maana WAMEOKOKA na tetemeko! Hata sasa Bwana Yesu analia mbinguni kuwaombea Mitume, Manabii, Wainjilisti, Wachungaji, na Waalimu ili waende kuvunja miamba mshapo, miamba tabaka, miamba moto , ili apate kujenga MNARA WA WOKOVU, hadi paradiso. HALELUYA!

***" Na malaika mwingine akaja akasimama mbele ya madhabahu, mwenye chetezo cha dhahabu,akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na MAOMBI YA WATAKATIFU WOTE juu ya madhabahu ya dhahabu, iliyo mbele ya kiti cha enzi. N amoshi wa ule uvumba ukapanda mbele za Mungu pamoja na MAOMBI YA WATAKATIFU, kutoka mkononi mwa malaika. Na huyo malaika akakitwa kile chetezo, akakijaza MOTO WA MADHABAHU, akautupa juu ya nchi, kukawa RADI NA SAUTI NA UMEME NA TETEMEKO LA NCHI." [ UFUNUO 8:3-5]***

Kwa kanisa la Tanzania Mungu amesikia MAOMBI YA WATAKATIFU, na kila jambo linalotokea Tanzania limekwisha pelekwa katika madhabahu ya Mungu kwenye kiti cha enzi na MALAIKA WA HABARI! Wapo watanzania wanafikiri MUNGU HAONI KILA UOVU UNAOENDELEA KATIKA NCHI YETU, KATIKA VYAMA VYA SIASA, KATIKA WIZARA, KATIKA SEKTA ZA UCHUMI WA NCHI, KATIKA TAASISI ZOTE ZA SERIKALI. Na wengine wamekata tamaa kuwa labda WEZI NA MAHARAMIA WALIOUZA NCHI NA MALIASILI ZAKE KWA SHETANI, wataendelea kufanya hivyo milele. Ndugu msomaji,





naomba ujue kwamba VILIO, MISIBA NA MAOMBOLEZO JUU TAIFA HILI BILA KUJALI KABILA, DINI WALA ITIKADI YA CHAMA CHOCHOTE, VIMEFIKA MBINGUNI KWA MALAIKA WALIOKO TANZANIA. MALAIKA HAWA TUMEWAOMBA KUFANYA OPERESHENI MAALUMU KWA TANZANIA NA MUNGU AMESIKIA, AMEKWISHA MRUHUSU MALAIKA ALIYEPELEKA MAOMBI KATIKA MADHABAHU YA MBINGUNI KWA CHETEZO, KIMEJAA MOTO WA MADHABAHU! AMEKWISHA KIRUSHA NA HUO MOTO WA TETEMEKO LA TANZANIA, ASOMAYE NA AFAHAMU. KWA NINI? KWA SABABU TATIZO LA KUYUMBAKWAMAISHAYAWATANZANIAWALIOCHOKA, WALIOCHAKAA NA KUFANYWA MASIKINI UMEMGUSA MUNGU!

Maombi yangu ni kuwa moto huu uje haraka uchome roho ufisadi, UCHOME ROHO YA RUSHWA, uchome roho ya uchawi, uchome roho ya sanamu, uchome roho ya uongo, uchome roho ya wizi wa fedha za watanzania, uchome roho ya ulevi, uchome roho ya woga, uchome roho ya kutoamini, uchome mioyo ya jiwe, uchome machukizo, uchome uzinzi, uchome mapepo na mashetani yanayotumiwa na kiongozi yeyote, uchome vyama vya kipepo, uchome minara ya kipepo, uchome mikataba ya mapepo iliyowaingiza watanzania kwenye matatizo ya kiuchumi, uchome roho ya umasikini, uchome roho ya ujinga na ubumbuazi juu watanzania, uchome kitambaa cheusi kilichowafunga macho watanzania wapate kuona, uchome roho ya kutojali maisha ya watanzania, uchome ya roho ya kufuja mali za taifa, uchome roho ya ulimbukeni, roho ya ubadhilifu, roho ya wivu, roho ya tamaa KATIKA JINA LA YESU!

TENGENEZA JESHI MAALUMU BABA WA MBINGUNI, HAO MALAIKA WALIO HODARI WA VITA ILI WATIMIZE MAPENZI YAKO TANZANIA. TENGENEZA JESHI BWANA, LA MALAIKA WA HUKUMU, WAFANYE MAPINDUZI YA KIROHO TANZANIA! OH! TUKUMBUKE TANZANIA TUNAKUSIHI, KWA HABARI YA WOKOVU, KWA HABARI YA MAJI, KWA HABARI YA MAFUTA, KWA HABARI YA VYAKULA NA KWA HABARI YA HUDUMA MBALIMBALI ZA JAMII! MALI ZETU ZIMEUZWA, MADINI YETU YANAUZWA, UTAJIRI WETU UMEUZWA, HATUNA KIMBILIO LINGINE ILA WEWE BWANA! TUMEWATEGEMEA VIONGOZI KWA MIAKA ZAIDI YA AROBAINI TANO SASA, KUMBE TULIKOSEA, EE BWANA YESU UTUSAMEHE KUWATEGEMEA WANADAMU, MAANA IMEANDIKWA AMTEGEMEAYE MWANADAMU AMELAANIWA! TUONDOLEE LAANA HII JEHOVA SHAMAH! WATENGE WATANZANIA NA UMASIKINI, WATENGE WATANZANIA NA ROHO YA KUABUDU MASHETANI, TENGA NURU NA GIZA LILILOFUNIKA NCHI YA TANZANIA, KATIKA JINA LA YESU KRISTO. AMINA!



# SURA YA KWANZA

## SAFARI YA KWENDA KWENYE MAOMBI

***“Baada ya maneno hayo yapata siku nne, aliwatwaa PETRO NA YOHANA NA YAKOBO, akapanda mlimani ili KUOMBA. Ikawa katika KUSALI kwake sura ya uso wake ikageuka, mavazi yake yakawa MEUPE, YAKIMETAMETA.”*** [LUKA 9: 28-29]

***“Kisha Yesu alipandishwa na ROHO nyikani, ali AJARIBIWE NA IBILISI. AKAFUNGA SIKU AROBAINI mchana na usiku, mwisho akaona njaa. MJARIBU akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, IMEANDIKWA, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila NENO litokalo katika kinywa cha MUNGU.”*** [ MATHAYO 4;1-4]

Maombi ni mazungumzo kati ya Watu na Mungu au Kati ya wasioamini na shetani. Maombi ni mkutano wa kivita ambao wajumbe wake ni wakristo waombao na Mungu; Mungu ndiye mwandaaji wa mkutano; anayesaini vita kwa Jina la Yesu; ndiye aliyekabidhi vifaa vya jeshi la maombi na ndiye anayeongoza vita kwa Roho wa Maombi. Katika vita vyote viwe vya kimwili au vya kiroho, lazima kuna sauti za kivita kwa sababu ya makombora yanayrushwa kwa rada ya kufyatulia; lazima kuna TETEMEKO LA VITA KWA SABABU YA SILAHA ZA KUJIAHAMI NA MAANGAMIZI. Silaha za kujihami ni aina ya silaha zinazompiga adui ili

kulinda jeshi na raia wa ufalme unaopigana. Silaha za maangamizi ni silaha ambazo hutumiwa na jeshi kulipua ngome ya adui pale alipopiga kambi yake ambako kuna jeshi la adui na silaha za kijeshi. Kwenye ngome ya adui ndipo mipango yote hufanyika ili kuivamia kambi ya mpizani wake. Wanajeshi waopigana na adui wana lugha maalumu ya kijeshi inayotumika katika mawasiliano ya kijeshi, na wanaishi kama wanajeshi, wanaongea kama wanajeshi na wanatembea kama wana jeshi.

Maombi ni MKUTANO WA KIFALME, kati ya MFALME NA WAFALME WADOGO PAMOJA NA WATU WENGINE KATIKA UFALME WAKE. Maombi ni safari ya kutoka katika ENEO LA CHINI KWENDA JUU KATIKA ULIMWENGU WA ROHO; KUTOKA DUNIANI KWENDA KATIKA KITI CHA MFALME WETU ALIPO. KWA SABABU SISI TUKO CHINI YA UFALME WAKE, NDIYO TUNAPASWA KUOMBA APOINTIMENTI YA KUKUTANA NAYE, KATIKA HEKALU LA KIFALME LILILOKO MBINGUNI. Mtu yeyote anapoanza kumtafuta Mungu kwa maombi kuna kusudi la kumtafuta; KABLA HUJAFIKA KATIKA GETI LA KUINGIA MAHALA PATAKATIFU PA PATAKATIFU KWA AJILI YA MKUTANO NA MFALME KUNA NGAZI NYINGI INABIDI UZIPITIE KUPELEKA MSTAKABARI WA MAOMBI. Tafakari mistari hii :

***" Unikumbushe; na tuhojiane; eleza mambo yako, upate kupewa haki yako." [ ISAYA 43:26]. Mtafuteni BWANA, maadamu anapatikana, MWITENI, maadamu yu karibu. " [ ISAYA 55:6]***





## Hatua za safari kupeleka Maombi kwa Mfalme wa Wafalme

Kabla ya kufanya mkutano na Mungu katika Ikulu yake Mbinguni unahitaji kufanya maandalizi ya kuomba siku maalumu na wakati maalumu wa kuongea naye. Wakati mwingine Mfalme mwenyewe anaweza kukupa ishara kwamba anataka mzungumze kwenye mkutano. Iwapo Mfalme anakuita uingie ilkulu, lazima kusitisha kazi zote ambazo ulikuwa unazifanya, na kuanza safari ya kwenda ikulu, mfanye mazungumzo. Hakuna ufalme wowote usiyo na utaratibu, Mungu katika ufalme wake ana utaratibu na mipango mikubwa na tofauti na mipango ya wafalme wa duniani. Biblia inasema mipango ya Mungu iko juu sana, kama ambavyo mbingu ziko mbali na dunia, kama tunavyosoma katika mistari hii:

***" Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, mawazo yangu kuliko mawazo yenu." [ ISAYA 55:8-9]***

Mbinguni ni juu sana na utukufu unapafunika, sisi tupo chini, tunahitaji kuandaa safari katika ulimwengu wa Roho ili kwenda kukutana na MFALME WA WAFALME, MFALME WA AMANI, MSHAURI WA AJABU, YESU KRISTO, MASIHI! AMESEMA ATATUONYESHA NJIA TUTAKAYOIENDEA, ATATUSHAURI NA JICHO LAKE LITATUTAZAMA. ANATUALIKA KATIKA MKUTANO WA MAOMBI, NA KUSEMA, NJOONI KWANGU NYOTE MLIYOLEMEWA NA MIZIGO YA DHAMBI NAMI NITAWAPA PUMZIKO! ANASEMA NIITENI NAMI NITAKUITIKIA

NITAKUONYESHA MAMBO MAKUBWA MAGUMU USIYOYAJUA! TUMEONA MAMBO MADOGO, LAKINI YALE MAKUBWA YANAPATIKA KATIKA MKUTANO WA MAOMBI. KWAHIYO MFALME ANAKUITA UENDE KUONANA NAYE HARAKA, UNANGOJA NINI?

UNAPOSITASITA NA KUCHELEWA, ANAKWENDA KUTUMA TETEMEKO, KWA ISHARA HII LAZIMA UTAKWENDA KWA NGUVU! ANAANDAA MALAIKA ILI WAKUKAMATE KWA NGUVU UENDE KWENYE MKUTANO, ANASUBIRI MUONANE, YEYE NI MFALME LAZIMA UTII! ACHA KUKIMBIZANA NA MKATE, ACHA KUKIMBIZANA NA MAISHA, ACHA KUANGAIKA NA MAISHA YAKO! MAISHA NA NAFSI YAKO NI MALI YA MUNGU! ANAPOSEMA NJOO, NENDA, ANZA SAFARI SASA! MFALME ANASUBIRI KATIKA KITI CHA ENZI, ANATAKA KUOMBA NA WEWE; YEYE AMEISHAJUA MATATIZO YANAYOKUKABIRI; NDIYO MAANA ANAKUITA AKUPE MAELEKEZO YA KUELEKEA UFUMBUZI WA MATATIZO, ADHA NA MISIBA ISIYOISHA! TANGU UMEANZA KUANGAIKA NA MAISHA HUKUNA JIPYA, KILA SIKU MATATIZO YANAONGEZEKA! BADO HUJASHITUKA KUMWENDEA MFALME WA AMANI? UNAKWENDA KWA WAFALME WA GIZA WEWE! NDIYO MAANA UNASHINDWA KWENDA KWENYE MKUTANO WA MFALME WA WAFALME! UNAOGOPA ATAKUULIZA ULIKUWA WAPI? KWA TAARIFA ANAJUA UNAKOKWENDA KILA WAKATI KUTAFUTA USHAURI! ANAKWENDA KUMPIGA MSHAURI WAKO KWA TETEMEKO KUU, MAANA AMETWAA UTUKUFU WAKE! UTUKUFU WAKE HAUGAWANYIKI, WALA HASHIRIKI UTUKUFU WAKE NA WANADAMU! UTUKUFU WAKE NI WA SHEKHINA. TOKAANZA SAFARI YA KWENDA KWA MFALME, KATIKA HATUA HIZI NINAZOKULETEA!





Sasa naamini unatamani kuanza safari ya kulekea kwenye mkutano na Mungu, ili upate kuzungumza naye, kwa habari ya maisha yako. Sasa nakutangazia kuwa safari hii ina hatua kadhaa ili upate kufika katika ikulu ya Mbinguni, hatua hizi ziko mfano wa RANGI SITA ZA UPINDE WA MVUA. Kumbuka Mungu alipofanya agano na NUHU aliweka upinde wa mvua kuwa ishara kwake na vizazi baada yake, kwamba Mungu hataigharikisha nchi tena, BAADA YA GHARIKA LA SIKU 40. Hadi leo ndugu msomaji unauona upinde wa mvua ukiwa na RANGI SITA NDANI. Rangi hizi zinatupa pia maelezo ya hatua ya kumfikia Mungu tunapoanza kumtafuta, hebu tuanze safari sasa hatua kwa hatua kwenda kwa mfalme kwa njia ya maombi, hizi ni ngazi kupafikia mahali pa mkutano, anza kupanda ngazi kama ifuatavyo.

## Hatua ya kwanza: Rangi ya Udongo au Njano:

Rangi hii unapoina inawakilisha roho ya mwanadamu, iliyoko ndani ya mwili. Maana mwanadamu ameumbwa katika nafsi ya MWILI, NAFSI NA ROHO. Mwili umetokana na udongo, roho imetokana na Mungu. Katika Mwili huu matendo yake yanapingana na Roho. Matendo ya mwili ni ya dhambi na matendo ya Roho ni UZIMA. Matendo ya mawili ni ya kufisha, bali matendo ya roho ni ya kuuisha. Katika mwili pekee huwezi kumwona Mungu, ambaye ni ROHO. Lazima uanze safari ya kutoka mwilini kwenda Rohoni, ili uanze kusafiri kuelekea katika ulimwengu wa roho, ULIMWENGU WA ROHO WA MUNGU. Naomba sasa upande ngazi ya kutoka kwenye udongo na upande katika hatua ya inayofuata uanze kwenda na kutembea katika roho ya maombi. Mungu tayari amekupulizia Roho

Mtakatifu ili mwili uliokufa kwa sababu ya dhambi uwe huu:

***" Bwana Mungu akafanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akapulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai."[ MWANZO 2:7]***

## Hatua ya pili: Rangi ya Kijani

Rangi ya kijana inawakilisha uumbaji wa Mungu juu nchi. Uumbaji wa Mungu unakuaminisha kuwa yupo Muumbaji ambaye ndiye mfalme, na kwamba nchi na viijavyo ni mali ya Mfalme. Unapoamini kwamba Mungu yupo, unaweza kwenda kuonana naye katika Ulimwengu wa Maombi. Huwezi kumwendea Mungu bila imani kuwa yupo, na wakati mwingine unaweza kuona ugumu kwenda kukutana na Mfalme usiyemwamini. Katika bendera ya Tanzania utaona hii rangi inawakilisha mimea na maliasili; katika mifumo ya safari, rangi hii hutumika katika taa za kuongoza magari barabarani, maana yake inapowaka taa ya kijani inakupa ruhusa kuendelea na safari. Kibiblia Mungu alituaminisha kwa kuumba mbingu na nchi kwa muda wa siku sita na siku ya saba akapumzika; HADI LEO SIKU YA SABA INAITWA SABATO. Sabato ni siku ya kumwabudu na kumsifu Mungu; NI SIKU YA MAPUMZIKO YA TAIFA LA MBINGUNI. Siku ya sabato siyo siku ya kuangaika na kazi za kaizari. Unaweza kutafakari mistari hii:

***" Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia zaeni, mkaongezeka, mkaijaze nchi, na kuitiisha, mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. MUNGU AKASEMA, TAZAMA, nimewapa kila mche utoao***





***mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu; na chakula cha kila mnyama wa nchi, na cha kila ndege wa angani, na cha kila kitu kitaambacho juu ya nchi, chenye uhai; majani yote ya miche, ndiyo chakula chenu; ikawa hivyo. Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. Ikawa jioni na asubuhi, SIKU YA SITA." [ MWANZO 1:28-31]***

## Hatua ya tatu: Rangi Nyekundu

Rangi hii ni alama inayowakilisha DAMU YA YESU inayobeba Roho wa Kristo. Hatua inayofuata baada ya kuanza safari ya kuzungumza na Mungu, lazima Damu ya Yesu ishuhudie. Damu ya Yesu inanena mema juu yako, inasafisha dhambi na uovu; inakuandaa na kukutakasa siku saba kabla ya kukutana na Bwana wa Majeshi, Bwana wa maombi; kama linenavyo agano la kwanza. Musa naye siku ambayo ilikuwa ni kukutana na Bwana katika Hema au katika mlima, Mungu alikuwa akimpa agizo la kulitakasa kusanyiko kwa muda wa siku saba kabla ya kukutana na Mungu katika wingu. Damu ya Yesu inakuleta katika upatanisho wa mafarakano yaliyokuwepo kati yako na Mungu katika Kristo Yesu. Inakupa kibali katika Agano la Damu ya kwenda kuonana na Mungu; Ukiwa ndani ya agano, Mfalme ametoa AHADI, MASHARTI NA MHURI UMEPIGWA KWA ROHO MTAKATIFU. Sasa unahesabiwa HAKI [JUSTIFIED TO SEE HIM], na malaika wanahakikisha mkataba unalindwa na kzingatiwa wakati wote. Sasa hii ni kama hati ya kusafiria, imegongwa viza na mhuri kwa Damu ya Agano, na Mfalme mwenyewe amekupa kibali KUONANA NAYE, MPATE KUZUNGUMZA. Hakuna uwezakano wa kusafiri kwenda katika nchi yoyote

bila hati ya kusafiria na viza inayotolewa katika ubalozi wa nchi hiyo, kulingana na taratibu za uhamiaji za kimataifa. Ukishapokea agano la Damu, umeruhusiwa kuingia TAIFA TEULE, TAKATIFU LA MBINGUNI; Kama tunavyosoma katika waraka wa Petro kwenye mistari hii:

***" Bali ninyi ni uzao mteule, ukuhani wa KIFALME. TAIFA TAKATIFU, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nru yake ya jabu; ninyi mliokuwa kwanza si TAIFA, bali sasa ni TAIFA LA MUNGU; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema. " [ 1 PETRO 2: 9-10]***

Baada ya kupata kibali cha kuingia taifa teule la Mungu, kinachofuata ni kuchukua chombo cha safari cha kuruka kama ndege kuelekea juu kwenda kwa MFALME katika ulimwengu wa roho.

## Hatua ya nne: Rangi ya Bluu

Chombo cha kuruka kwenda juu katika ulimwengu wa roho kinawakilishwa na roho ya TAI, ambayo inawakilishwa na rangi ya bluu. Roho ya tai ni mfano wa Roho wa maombi, kuruka mbali sana kwenda juu katika ulimwenguwa roho upate kukutana na Mfalme wa Maombi, Bwana Yesu. Huwezi kumuona MFALME bila kuwa na roho ya tai, kwa sababu roho ya tai inakupa mbawa za kuruka na nguvu za kuruka kama tai. Tai ni ndege ambao huruka sana kwenda juu katika hali ya hewa ya ubaridi, ambapo hakuna joto na ndege wengi hawawezi kufika. Jiografia inasema jinsi unavyoruka umbali mrefu kwenda juu, ndivyo joto linapungua kutoka usawa wa bahari. Na ndege kama





mashine za kuruka kwenda juu, zinaporuka umbali mrefu ndivyo zinapata kubalansi mabawa yake. Biblia inaongelea juu ya roho ya tai katika mistari hii:

***" Haya vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka, bali wao wamngojeao BWANA watapata nguvu mpya; WATAPANDA JUU KWA MBAWA KAMA TAI; watapiga mbio, wala hawatachoka….."[ ISAYA 40: 30-31]***

## Hatua ya tano: Rangi ya Zabibu

Unapofika malango ya Mbinguni, baada ya kuruka kwa umbali mrefu kutoka duniani, kabla hujaingia katika hekalu la Bwana ambamo kuna sanduka la agano hadi leo, lazima upokee ROHO YA SIMBA WA KABILA LA YUDA. Bila roho ya simba huwezi kumuona MFALME, kwa sababu hekaluni kunatisha. Ukitazama mbinguni kuna viumbe wa ajabu karibu na kiti cha enzi. Kuna malaika wa aina nyingi, wenye uhai wa nne ambao wana macho kila upande, magari ya moto ya kule na wengine wengi ambao siwajui. Mungu ni moto hulao kumuona uso kwa uso anatisha, hata Musa aliambiwa Mungu anatisha. Roho ya simba wa kabila la Yuda, ni Roho ya Kristo inakupa mamlaka ya kumuona MFALME WA WAFALME. Biblia inaonyesha utiisho wa roho ya simba katika mstari huu:

***" SIMBA amekwisha kunguruma, ni nani asiyeogopa?....." [ AMOSI 3:8 ]***

## Hatua ya sita: Rangi ya Nyeupe

Rangi nyeupe inawakilisha ROHO YA UTUKUFU WA MUNGU, ULE UTUKUFU WA SHEKHINA. Utukufu wa

Mungu au mfano mwingine. Katika kiti cha enzi,utukufu wa Mungu ni mkuu sana, kabla hujakaribia katika maombi inakupasa kutimiza haki zote za kukukaribia. Katika agano la kale, mfano wake ni madhabahu katika hema la kukutania, ambapo palikuwa na sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaitwa MAHALI PATAKATIFU NA SEHEMU YA PILI, ILIYOTENGWA KWA PAZIA, PANAITWA PATAKATIFU PA PATAKATIFU. Sehemu ya kwanza, watu wote walikaribia kutoa sadaka mbalimbali ikiwa pamoja na dhambi. Sehemu ya pili KUHANI NDIYE ALIRUHUSIWA KUINGIA MARA MOJA KWA MWAKA KUTOA SADAKA ZA DHAMBI. KABLA KUHANI HAJAINGIA KUTOA SADAKA YA DHAMBI, ALIPASWA KUJITAKASA SIKU SABA; KISHA ALIFUNGIWA KENGERE MGUUNI, ILI KWAMBA AKIWA HAJAJITAKASA NA MUNGU AKAMUA KWA SABABU YA MAKOSA YAKE MWENYEWE, BASI WATU WAKISIKIA KIMYA HAKUNA KENGERE INAYOLIA, WANAJUA AMEKUFA. KWA SABABU PANATISHA HAKUNA MTU MWINGINE ALIRUHUSIWA KUKARIBIA, WALICHUA KAMBA ILE NA KUVUTA MWILI WA MAITI ILE ILI WAENDE KUIZIKA.

Lakini Bwana Yesu alipokuja na kufanyika dhabihu kwa ajili ya watu wote, lile pazia lilipasuliwa VIPANDE VIWILI kutoka juu hadi chini kwa tetemeko la msalaba. Vipande viwili vinasimama badala ya AGANO JIPYA NA AGANO LA PILI; DHABIHU YA YESU KRISTO PALE MSALABANI IKATETEMESHA MBINGU, NCHI NA KUZIMU, NA IKAPOKOLEWA KATIKA HEKALU LA MBINGU. MAPINDUZI HAYA YAKASABABISHA KUZALIWA KWA AGANO JIPYA, LA DAMU YA YESU, MBALO LILIFANYWA NA YESU MWENYEWE. TANGU WAKATI HUU, KILA





MMOJA ANARUHUSIWA KUKARIBIA KITI CHA ENZI NA REHEMA KWA TOBA, HOFU NA KUTETEMEKA MBELE ZA MUNGU WETU, UWE MYUNANI AU MYAHUDI, MATAIFA AU MWENYE HAKI, UNAYEAMINI AU USIYEAMINI KATIKA JINA LA YESU! LAKINI LAZIMA MASHARTI YA KUINGIA PALE KWA UTAKASO, YAZINGATIWE; HUWEZI KUKARIBIA KITI CHA ENZI BILA UTAKASO WA MWILI NA ROHO. Unaweza kukaribia kiti cha enzi kwa maombi; na hapa ndipo kuna majibu yote ya MBINGUNI, DUNIANI NA KUZIMU.Tafakari juu ya mistari hii kuhusu tetemeko lilitokea YESU ALIPOTIMIZA HUDUMA YA MSALABA:

***"Na tazama, pazia la hekalu likapasuka VIPANDE VIWILI toka juu hata chini; NCHI IKATETEMEKA; miamba ikapasuka; MAKABURI YAKAFUNUKA; ikainuka MIILI MINGI YA WATAKATIFU WALIOLALA. nao wakiisha kutoka makaburini mwao, BAADA YA KUFUFUKA KWAKE, wakaingia MJI MTAKATIFU, wakawatokea wengi wengi. [Mathayo 27:51-54].***

Mfano mwingine wa Utukufu wa Mungu unaojihidhirisha wakati unapofika katika uwepo wa Mungu na kukaribia katika kiti cha enzi katika maombi, ni pale ambapo YESU aliwachukua, PETRO, YAKOBO NA YOHANA wakapanda kwenye mlima mrefu KUOMBA. Unaweza kusoma habari hii katika mistari hii:

***" Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani; akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukangaa kama jua, MAVAZI YAKE YAKAWA MEUPE KAMA NURU. [Mathayo 17:1-3]***

***" Baada ya maneno hayo yapata siku nne, aliwatwaa PETRO NA YOHANA NA YAKOBO, akapanda mlimani ili KUOMBA. Ikawa katika KUSALI kwake sura ya uso wake ikageuka, mavazi yake yakawa MEUPE, YAKIMETAMETA." [LUKA 9: 28-29]***

Katika taarifa ya injili ya LUKA hapo juu inaweka bayana kuwa, MWOMBAJI ANAPOKARIBIA KITI CHA UTUKUFU CHA MUNGU, KWANZA SURA YAKE INAGEUKA, PILI MAVAZI YAKE YA KIROHO NA KIMWILI YANAKUWA MEUPE NA TATU YANAMETAMETA. RANGI NYEUPE INAWAKILISHA ROHO YA UTAKATIFU. NDUGU MSOMAJI WANGU NAPENDA NIMALIZIE SOMO HILI, JUU YA ROHO ZINAZOSIMAMA BADALA YA RANGI MBALIMBALI, KWAMBA HATIMA YA MAOMBI YOYOTE PAMOJA NA TETEMEKO, PAMOJA NA MAJIBU YOTE, NI ROHO YA UTAKATIFU. KUMBE MAOMBI NI NJIA KUFIKIA UTAKATIFU.

**Wakati wa kuongea na Shetani katika Maombi**

Wakati mwingine mkristo katika ngazi ya MWAMINI, MWANAFUNZI AU MTUMISHI anaweza pia kuongea na shetani. Wakristo wengi hawapendi kuongea na mapepo na mashetani, lakini Wakristo imara katika kiwango cha juu wanaweza kuongea na shetani na mapepo yake katika maombi yoyoye, lakini hasa katika maombi ya kufunga. Bwana Yesu aliongea na shetani alipokuwa katika maombi ya kufunga siku 40 akiwa nyikani, kwa NENO LA MUNGU, kama tunavyosoma katika mistari hii:

***" Kisha Yesu alipandishwa na ROHO nyikani, ali***





***AJARIBIWE NA IBILISI. AKAFUNGA SIKU AROBAINI mchana na usiku, mwisho akaona njaa. MJARIBU akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, IMEANDIKWA, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila NENO litokalo katika kinywa cha MUNGU."[ MATHAYO 4;1-4]***

Roho Mtakatifu anaweza kukuletea roho ya shetani ili tu siyo kuiamuru, bali mzunguze kwa NENO LA MUNGU. Mkumbushe shetani habari zilizompata kule mbinguni, jinsi ambavyo alipigwa, na kufukuzwa mbinguni, pamoja na malaika zake. Roho ya Maombi ni Roho wa Mungu, anaweza kuongea ndani ya roho yako pamoja na shetani, kumweleza mapenzi ya Mungu. Maana shetani yeye hutafuta kudanganya, kushawishi kwa uongo, kulitukana Neno la Mungu, Kulihukumu Neno, kuharibu uumbaji wa Mungu na kisha kupotosha ukweli, na hatimaye kuuwa. Mitume, Manabii, Wainjilisti, Wachungaji na Waalimu, tunahitaji kuongea na shetani ana kwa ana katika Roho ya maombi; ukimweleza kilichompata mbinguni, Kalivari pale msalabani kisha kumwonyesha hatima yake na hukumu ya mwisho katika ziwa la Moto wa Jehanamu; LAZIMA ATATETEMEKA NA KUKIMBIA.

***" Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa WAKIMWOMBA Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza. Ghafula pakawa TETEMEKO KUU LA NCHI, hata misingi ya gereza IKATIKISIKA, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vya wote vikalegezwa." [MATENDO 16:25-26].***

Tetemeko linalotokea kwa kufunga na kuomba ni kubwa kiasi kwamba, hadi nchi inatetemeka, na misingi ya GEREZA ZA KIMWILI NA KIROHO INATIKISIKA. Vifungo vyote vya shetani na mshetani wake huvunjika na kuachilia, milango ya upenyo wa kiroho na mwili kama WOKOVU, KUKOMBOLEWA, KUACHWA HURU DHIDI YA VIFUNGO VYA SHETANI, MILANGO YA KIUCHUMI HUFUNGUKA, MILANGO YA FURAHA HUFUNGUKA, MILANGO YA KUOA NA KUOLEWA HUFUNGUKA, MILANGO YA BIASHARA HUFUNGUKA, MILANGO YA KUSOMA HUFUNGUKA, MILANGO YA HUDUMA HUFUNGUKA, MILANGO YA INJILI HUFUNGUKA, MILANGO YA SAFARI ZA UMISHENI HUFUNGUKA. Kwa nini? Kwa sababu kuna nguvu ndani ya Maombi inayosababisha TETEMEKO LA KIROHO NA KIMWILI JUU YA SHETANI, ROHO MTAKATIFU HUWAFUNIKA WAOMBAO, NA KISHA HUWAPA NGUVU ZA KUHUBIRI NJILI KWA UJASIRI, ISHARA NA MIUJIZA MINGI. Roho ya Simba wa kabila la Yuda huwafunika na Roho ya Tai huwainua kupeleka injili BILA KUJALI VIKWAZO. Kama tunavyosoma katika mstari ufuatao:

***“ Hata walipokwisha KUMWOMBA Mungu, mahali pale walipokusanyika PAKATIKISWA[ NA TETEMEKO], wote wakajaa ROHO MTAKATIFU, WAKANENA NENO la Mungu kwa ujasiri.” [ MATENDO 4:31 ]***

Shetani anaogopa maombi na anatafuta kuwanyanganya silaha wakristo wengi hawajui, maana anajua inabatilisha mipango aliyonayo kwa Kanisa la Mungu na taifa. Ukitaka kujua shetani anavyopinga maombi fatilia vikundi ya





WAOMBAJI, jinsi vinavyopingwa na Wachungaji ,Wakuu wa dini na Wakuu wa Giza. Mimi nilipoitwa na Mungu kwenye huduma ya maombi, Mungu alinipa watu watano wa kuomba nao, TETEMEKO LA MAOMBI LILIPOANZA, MAPEPO YAKALIPULIWA, VIPOFU WAKAONA, VIWETE WAKATEMBEA, WALIOFUNGWA WAKAFUNGULIWA, VIZIWI WAKASIKIA; NDIPO MCHUNGAJI ALIINITA AKANIAMBIA NATAKA UACHE MAOMBI. NILIMJIBU KUWA MCHUNGAJI KUNIZUIA MAOMBI NI SAWA NA KUNIAMBIA NIACHE WOKOVU. Ndipo nilifunuliwa kumbe shetani anaweza kumtumia mtu yeyote, mwamini, mkristo au mtumishi wa Mungu ili aweze kupinga huduma. Ndipo nikakumbuka Bwana Yesu alipokuwa anamkemea shetani ndani ya Petro, alipomwambia RUDI NYUMA YANGU SHETANI. Kumbe alimwona shetani ndani ya Petro aliyetaka kuzuia HUDUMA YA UKOMBOZI YAANI WOKOVU. Ni kweli bila maombi ndugu msomaji wangu, huwezi kuendelea na wokovu! Wokovu bila maombi, lazima utarudi nyuma, bila kujali wewe ni Mtume, Nabii, Mwinjilisti, Mchungaji na mwalimu.

Tukirudi katika mstari wetu hapo juu, ni vigumu watu kuokoka na kufunguliwa kama HAKUNA MAOMBI, maana ufalme wa giza HAUJATIKISWA KWA TETEMEKO. Ufalme wa shetani hukitikiswa, huachilia watu wa Mungu, ndipo Roho Mtakatifu huwatawala. Roho Mtakatifu akitawala, ndipo watumishi wa Mungu hupokea Roho ya simba wa kabila la Yuda kuhubiri kwa ujasiri. Roho mtakatifu huwafunulia watumishi wake waombao, na kuwapa maelekezo jinsi gani wataifanya kazi ya Mungu. Kwa sababu katika maombi tunapewa maelekezo ya kufanya kazi na jinsi kupata maarifa ya kutatua matatizo ya watu.